***Baadaye ndipo nilipata wazo kwamba ninaweza kufanya uzinduzi wa kitabu kwa njia ya kuitisha harambee na kisha fedha itakayopatikana kupitia hiyo harambee itumike kujenga makanisa vijijini***. Wazo hili lilipokuja ndipo nikakumbuka kuwa kuna watu waliwahi kunishauri kuwa huduma ya kujenga makanisa iwe endelevu badala ya kuishia kwenye ujenzi wa lile kanisa la kwanza.

Ni wakati huu sasa ndipo nilipata mzigo mkubwa sana juu ya huduma hii na Mungu akanionesha jinsi huduma itakavyoenda. Kwanza alinionesha kuwa uzinduzi wa kitabu utafana sana na tutapata fedha nyingi na kwamba atainua watu wengi watakao toa fedha kwa ajili ya huduma hii. Hata kuna watu walio nje ya kikundi hiki ambao waliota ndoto kuhusu tukio la uzinduzi wa kitabu na walioneshwa limekuwa tukio kubwa sana. Wakati wote wa maandalizi ya uzinduzi wa kitabu Roho Mtakatifu aliniongoza kwa kila hatua. Roho Mtakatifu akanionesha kuwa wakati wa uzinduzi wa kitabu tutazindua rasmi na kuwekwa wakfu huduma ya kujenga makanisa vijijini. *Wazo la kualika watu, kuandaa fomu ili kuwashirikisha kuchangia ujenzi wa makanisa vijijini lilikuja tu akilini mwangu na sikuamini kwa haraka haraka kama lingezaa matunda. Mungu alithibitisha kuwa alikuwa pamoja nasi kwani tulipata fedha Zaidi ya mara mbili ya lengo la awali*. Jambo la ajabu zaidi ni kwamba zaidi ya 98% ya ahadi zote zilikusanywa tofauti na kawaida ya watu kuahidi bila kutoa. Jambo hili kwangu lilitosha kunithibitishia kuwa Mungu ameniambia kuwa niende kujenga makanisa na fedha zitatoka kwake.

Tangu wakati huo nikawa na uhakika juu ya huduma hii na nikapata mawazo mapana ya jinsi ya kufikiria na kuendesha huduma hii. Wakati huu ndipo nikapata maono ya kufungua akaunti ya benki kwa ajili ya kukusanya michango ya huduma na kuandaa katiba ya kikundi. Nilimshirikisha ***Mr. Elias Mushi*** juu ya wazo la kufungua akaunti ili itumike wakati wa uzinduzi wa kitabu na pia iwe akaunti ya moja kwa moja kwa ajili ya huduma ya Tujenge Nyumba ya Mungu. Tulishauliana na *Mushi* juu ya jina la huduma na jinsi ya kuandika Katiba ya kikundi kwa ajili ya kufungua akaunti na hatimaye tukafanikiwa kufanya hivyo.

Baada ya hapo tulishirikisha wanakikundi wote juu ya uanzishwaji rasmi wa huduma ya kujenga makanisa na nikawaomba wanakikundi kwa hiyari yao wenyewe waridhie kuanzishwa rasmi kwa huduma. Kwa bahati nzuri wadau wote sita (6) walikubali na pia tukapata wadau wengine watatu ambao ni *Mrs. Rose Ngitoria, Mr. Ernest Daudi na Mr. Nuhu Stanley*. Hivyo, hadi wakati tunazindua rasmi huduma pamoja na kitabu tarehe ***12 Mwezi Machi 2023,*** huduma ilikuwa na idadi ya washirika kumi (10). Siku ya uzinduzi pia tulipata mshirika mwingine ambaye ni ndugu *Anthony Elihudi* na baadaye wengine walioongezeka ni ndugu *Margreth Stephano, Glory Matemba, Mrs.Tunu Mwiru na Mr. Mwanzalima* na hivyo kufikisha idadi ya jumla ya watu kumi na tano (*15).*